

Mtumishi wa Mungu: Eng John James Ndindwa
**Subject:** NGUVU YA KIJANA KATIKA KANISA
Contact: Email; ndindwajohn@gmail.com | Cell: 0717 401 569 |
Episode: Mafundisho ya Vijana

*"1 Yohana 2:14 Nimewaandikia ninyi, akina baba, kwa sababu mmemjua yeye aliye tangu mwanzo. Nimewaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mna nguvu, na neno la Mungu linakaa ndani yenu, nanyi mmemshinda yule mwovu*

Utangulizi

## KIJANA: RASILIMALI YA MUNGU KULETA MABADIRIKO KATIKA UFALME WA MUNGU NA KUATHIRI JAMII KATIKA MTIZAMO CHANYA

**Kwa sababu ana Nguvu:**

*1 Yohana 2:14 Nimewaandikia ninyi, akina baba, kwa sababu mmemjua yeye aliye tangu mwanzo. Nimewaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mna nguvu, na neno la Mungu linakaa ndani yenu, nanyi mmemshinda yule mwovu*

Nishati ni kani inayowezesha kufanya kazi ama kufanya mambo yatendeke

Ili mambo yatendeke yanahitaji NGUVU. Kiwango cha MATOKEO huendana na NGUVU iliyotumika. Mungu amewekeza NGUVU kwa KIJANA.

UTUKUFU/FAHARI ya kijana yeyote ni NGUVU. Raisi wa tatu wa Israel aliwahi kusema, namnukuu "Fahari ya vijana ni nguvu zao, Na uzuri wa wazee ni kichwa chenye mvi" (Mithali 20:29). NGUVU iliyowekezwa kwa KIJANA ikitumika vizuri, hubadilisha hali ya eneo kiuchumi na kiroho. Kanisa ama jamii ikiwa na hali mbaya kiroho au kiuchumi, tutaanza kumwangalia KIJANA kwanza.

"……Nimewaandikia ninyi, vijana kwa sababu mna nguvu……" (1 Yohana 2:14). Mungu anataka tujue, "VIJANA TUNA NGUVU". Kama hatuzitumii nguvu hizi, si kosa la Mungu; ni kosa letu. *Kama hatuleti mabadiliko chanya kwenye jamiii inayotuzunguka, hilo ni kosa letu!.*

### AINA YA NGUVU ALIZONAZO KIJANA

Kuna aina ya nguvu zilizo kwa kijana. Kila kijana anapaswa kujua aina ya nguvu alizonazo; Baadhi yan nguvu hizo ni.

### 1. NGUVU YA MAONO

Nianze kwa kunukuu maneno ya hekima ya Raisi wa tatu wa Israeli, Mfalme Sulemani anasema "Pasipo maono watu huacha kujizuia…." (Mithali 29:18). Kwa kijana yeyote aliyejitambua tayari, anayejua ana nguvu ya maono HUJIZUIA!

1.1 Ni nguvu ya maono inayompa kijana kujiwekea mipaka. Neno la Mungu linasema "……vijana wenu wataona maono…." (Matendo ya mitume 2:17).

1.2 Nguvu ya maono kwa kijana humpa kuona maono, na maono humwekea mipaka. Vijana tukitumia nguvu ya maono iliyowekezwa kwetu na Mungu, kanisa la Mungu haliwezi kulia-lia uchumi mbaya; kanisa halina hela au mchungaji hana chakula. Tutaona wapi tunatakiwa tuwe, viwango gani ni stahili yetu!. Kanisa litainuka kiroho na kiuchumi.

## 2. NGUVU YA KUTUMIKA

Aliyeambiwa Neno hili ni kijana kwamba "Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako….." (Mhubiri 12:1). Vijana, tunamkumbuka Mungu kwa utumishi tulio nao kwake. Sisi ni vijana, tuna nguvu ya kutumika. Tunatumika katika maeneo yote, kuanza na kuhubiri, kufundisha mpaka kwenye mifuko yetu; tukijitoa kwa fedha zetu kwa ajili ya kazi ya Mungu. Neno la Mungu linasema " Lakini Samweli alikuwa akitumika mbele za BWANA, naye alikuwa kijana………" (1 Samweli 2:18).

## 3. NGUVU YA KUZALISHA

Waefeso 4:28 Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji. Mojawapo ya maeneo makubwa kwa wapentekoste magumu ni maisha ya wacha Mungu walio katika makanisa wanaomba sana huku umasikini ukiwaandama kwa kutokufanya kazi kwa bidii, kwa weledi, kujituma, kujitesa, kuhangaika ili Mungu abariki kazi ya mikono yao. Mungu wa walokole yuko kwenye jengo na hayuko katika majukumu yao ya uzalishaji. Hivyo wana Mungu anaishi kanisani na katika kazi hawi nao.

Kutoka 31:5 na kukata vito kwa kutiwa mahali, na kuchora miti, na kufanya kazi ya ustadi iwayo yote…Eliazari aliyeitwa na Mungu kwa kazi maalumu kwa weledi wake.

## MAMBO SABA YA MSINGI YA KUKUSAIDIA KUTAMBUA THAMANI NA NAFASI YAKO KAMA KIJANA MKRISTO: Change we need, Yes We can!

1. Ni vizuri ufahamu kwamba KABLA HAUJAZALIWA Mungu alishakujua na aliweka tayari KUSUDI, NYAKATI, na UWEZO ndani yako maalum kwa ajili ya KANISA.{Yeremia 1:5; Zaburi 139:13,15,16;}

**Maisha yamefichwa kwenye Muda na Nyakati**

Mhubiri 3:1 Kwa kila jambo kuna majira yake, Na wakati kwa kila kusudi chini ya mbingu.

Waefeso 5:16 mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu.

Wakolosai 4:5 Enendeni kwa hekima mbele yao walio nje, mkiukomboa wakati.

2. Licha ya uzuri mwingi ulioko kwenye UJANA, UJANA ni kipindi cha MPITO i.e. UMEPIMWA KWENYE MUDA na kwa hiyo basi UJANA HUPITA UPESI.{Mhubiri 12:1; Yohana 21:18;Matendo 17:26;Mhubiri 3:1,11}

3. Kijana ni KIUNGO MUHIMU SANA katika mwili wa Kristo yaani KANISA hivyo ni vema utambue thamani na nafasi yako katika kujenga na kuimarisha KANISA i.e. Mwili wa Kristo.{Waefeso 5:23; 1Korintho 12:27;Waefeso 4:12,16}

4. Udhaifu na Ulemavu wa KANISA LA LEO ni matokeo ya VIUNGO vingi kulala na kutofanya kazi ipasavyo, na hasa VIJANA. {Mithali 25:14 ;}

**Matatizo ya kanisa la sasa**

1. **Ulemavu:-** Kanisa halikui kwa idadi kwa sababu vijana wameishia kuimba majukwani na kwenye matamasha wakisakata viduku na hawahubiri mtaani.
2. **Kudumaa:-** Kanisa limedumaa kwa sababu maisha ya vijana ni shuhuda mbovu kwa walio nje, check mavazi yao, wanavyonyoa, ndoa zao, shuhuda zao, urembo kwa wadada kama makahaba, wanaimba wamevaa vipedo jukwaani, wamevaa suruali, transparent nk
3. **Dhaifu:-** kwa sababu vijana hawana nguvu ya kumtafuta Mungu awape uwezo wa kufundisha injili hai na yenye ufunuo, matokeo tuna makanisa yenye watu wengi *(wanaotegemea miungu watu inayopatikana maeneo Fulani na siyo)* wasio mjua Mungu na yasiyoweza kuyashinda malango ya kuzimu.

   *Mathayo 16:18 Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.*

4. **Jamii Umasikini:-** Vijana wengi wanaacha mashamba kulima na kwenda mjini kubeti na kucheza kamali, Ukienda baadhi ya maeneo kigoma, wamama ndio wazalishaji wa mazao na chakula cha familia na waume zao wanashinda kwenye pombe, (nenda sokoni utakuta wamama wengi)

5. Kijana anayeweza kuleta MABADILIKO kwenye KANISA ni Yule ambaye tayari ametambua thamani na nafasi yake *(mwili na nafsi yake)* kama kiungo katika MWILI wa KRISTO yaani KANISA, na anatumika katika kiwango na muda husika/sahihi {Yohana 4:34}

*1 Timotheo 4:12 Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi.*

6. Wala asimpe ibilisi nafasi

Waefeso 4:27 wala msimpe Ibilisi nafasi. Yakobo 4:7 Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia.

7.Kanuni ya kukimbia kwa habari ya baadhi ya vitu kama uvivu. Kanisa linatembea dunia inakimbia, vijana watembea utandawazi unakimbia sana. Lazima vijana wakimbie kwa habari ya kuutafuta utakatifu na haki ya Mungu na kuchapa kazi na umasikini utakimbia kwao.

Mwanzo 41:38 Farao akawaambia watumwa wake, Tupate wapi mtu kama huyu, mwenye roho ya Mungu ndani yake?